TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUTAFUTA KUMBUKUMBU REJEA ZOTE.

Kwa wale wanaoishi katika nchi zenye Serikali nzuri ambako kuna amani na utawala wa Sheria ni rahisi kusema kwamba hofu ni jambo unaloweza kupambana nalo. Pambana na hofu ni kauli mbiu ya siku hizi.

Katika miaka ya karibuni hata watu ambao wako katika nchi zenye amani wanakuwa wakijifunza inakuaje kuishi katika hofu mchana na usiku kwa sababu ya vita, mara nyingi vita vya mara kwa mara katika nchi zao. Kutokana na maafa ya asili kama matetemeko, volkano, mafuriko, maporomoko ya udongo wa milimani, pepo kali, vimbunga hutegemea wanaishi wapi katika dunia hii.

Hofu hii inakuja kutokana na kutokujua nini kitakutokea baadaye, kutokna na mashambulizi ya ghafla juu ya mali yako au kutoweza kujisaidia wewe mwenyewe, familia yako au rafiki unapotishwa. Matukio ya ghafla na mstuko wa ghafla unaweza kumpata kila mtu, lakini kile kilichosababisha somo hili kuandikwa hasa ni kutuonyesha namna ya kuangalia na kuishinda hofu iliyoshindikana kuondoka. Hofu tuliyonayo mchana na usiku kwa siku nyingi, majuma au hata miaka.

Kuna mifano ya wazi kabisa katika Biblia na sasa tunaweza kuisoma mifano hii pamoja ili kuona jinsi watu hawa walivyoathirika.

Kwanza kabisa katika Kutoka sura ya 14 mstari wa 10 ambapo watu wa Israeli waliookolewa katika utumwa katika nchi ya Misri, wanagundua kwamba wanafuatiliwa na majeshi ya Wamisri yanayotaka kulipiza kisasi. Bahari iko mbele yao na Wamisri nyuma yao, kwa hali iwayo yoyote ile waliogopa.

Mfano mwingine wakati huu ni kumbukumbu la Torati sura ya 28 mstari wa 63 hadi 67. Unaposoma maneno haya utaona kuwa yanaelezea hofu isiyoondoka. Mungu anawaambia watu wake kuwa hii itawatokea iwapo watamwacha na kuanza kuabudu Miungu iliyotengenezwa kwa mbao na mawe. Wayahudi walimwacha Mungu, na historia yao mpaka siku ya leo inajumuisha miaka mingi walioishi katika hofu kubwa. Katika Ujerumani, kati ya miaka ya 1939 na 1945, kati yao milioni 6 waliuawa kikatili kwa sababu tu walikuwa Wayahudi. Huu ni mfano wa kutisha wa kuishi katika hofu.

Hofu ni mbaya zaidi ikiwa kitu chenyewe hakifahamiki. Inaweza kuathiri makundi mazima ya watu. Hofu kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine katika mazungumzo. Linapotokea kwako, jambo la kwanza unaloweza kufanya kama mtu binafsi ni kutambua kile kinachosababisha hofu. Nani au nini kiwajibike. Baada ya hapo inawezekana kuona jinsi gani unaweza kufanya juu ya kile kinachosababisha hofu. Kuikana nyumba yako, Kijiji chako, familia yako na marafiki zako, inaonekana kuwa ndiyo njia pekee ya busara unaweza kuichukua.

Tangu kuanzishwa kwa Kanisa la Kikristo, wafuasi wa Yesu wamekuwa wakiteswa kama ilivyo kwa watu wengine. Wakati mwingine ilikuwa hivyo kwa sababu ya kuwa Wakristo, hata hivyo haikuwakatisha tamaa kuwa wanafunzi, badala yake walizidi kuwa na nguvu zaidi katika imani yao na utiifu kwa Yesu.

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinatuambia kuhusu kazi ya kuhubiri iliyofanywa na Mitume katika nchi za Kaskazini ya bahari ya Mediteraniani inaonyesha kwamba kila walikoenda walitishwa na makundi ya Wayahudi walioishi katika maeneo hayo.

Mitume walipigwa, walipigwa mawe hadi kufa na kutupwa katika magereza, lakini hatuoni kuwa waliogopa au kushindwa. Kinyume chake, mara nyingi Mungu aliwatuma Malaika wake kufungua milango ya magereza – Matendo sura ya 16 mistari ya 22 hadi 29. Hebu fikiria, Paulo na Sila kuumizwa kwao kulitokana na kupigwa hata wasiweze kulala, badala yake waliimba nyimbo za kumsifu Mungu (Labda kutoka katika Kitabu cha Zaburi).

Kutoka katika siku za mwanzo za Kanisa la Yesu Wanafunzi walijua ilikuwaje kuishi katika hofu, hata hivyo hawakuruhusu itawale maisha yao. Badala yake Yesu alikuwa mtawala shupavu wa maisha yao na kwa sababu yake hawakukatishwa tamaa kwa kuogopa. Mfano wake mwenyewe, kutoka siku ile ya kutisha, akiwa anajua kuwa katika muda mfupi watu wakatili wangefika kumkamata na kumchukua kwenda kusulubiwa hata hivyo aliwatia moyo wafuasi wake wa wakati ule na atendelea kufanya vivyo hivyo kwetu sisi leo.

Ni katika Injili ya Luka ambapo tunaweza kusoma hali ya wakati mgumu sana kwa Yesu sura ya 22 mstari wa 39. Sasa endelea kusoma mstari wa 44. Alijua kutokana na utabiri nini

kingemtokea na kwa kuwa alikuwa mtu, aliogopa. Hata hivyo kwa kuwa alikuwa Mwana wa Mungu, alijua kwamba kifo hiki cha maumivu makali ilikuwa ndiyo thamani ambayo ni lazima kulipwa kwa sababu ya dhambi za wanadamu. Kwa ushupavu alisimama mahali alipolala kifudifudi akiwa katika kuomba Baba yake na kuondoka mahali pale penye usalama ili kukabiliana na wale waliokuwa washitaki wake wa uongo na hatimaye kifo chake. Yesu hakuwahi kuwa ahidi wafuasi wake maisha yasiyo na matatizo na hofu bali alionyesha kuwa maisha tunayoishi hivi sasa ni utangulizi katika Ufalme wake. Baadhi ya Wafuasi wake watafariki kwa sababu ya kuwa Wakristo lakini katika shabaha yake Mungu hawatapotea au kusahauliwa. Katika siku ya ufufuko, wataamka katika Dunia pamoja na wale wengine ambao wameishi na kufa kwa amani.

Angalia katika maneno ya Yesu katika Luka sura ya 12 mistari ya 4 hadi 7. Katika maandiko haya kuzimu ni kaburi na wale ambao hawaukubali wito wa Mungu wa ukombozi watapumzishwa humo milele.

Ikiwa tutajikabidhi mikononi mwa Mungu kuweka imani yetu kwa muumba mwenye nguvu Mungu aliyetuumba na kutuweka katika dunia hii kwa makusudi yake ya ajabu sana.

Kutunyanyua juu ya athari za hofu tuna maneno ya kututia moyo kama yale yaliyo katika Waraka wa Paulo kwa Wakorintho sura ya 3 mstari wa 16. Msingi wa maisha yetu ni Yesu – mstari wa 11, kama tumebatizwa katika jina lake. Mistari ya 12 hadi 15 iko pale kutuonyesha wazi wazi kwamba ikiwa vitu vyetu vyote vimepotea lakini bado tuna imani, kwa hiyo bado tumeokoka katika makusudi ya Mungu.

Sasa na turudi nyuma katika kitabu cha Kutoka sura ya 14 na tuone kilichowatokea wana wa Israeli. Kumbuka kuwa daima walikuwa katika hali ya mashaka, walijikuta kati kati ya bahari ya Shamu na Jeshi la Wamisri yakiwajongea karibu.

Sasa angalia katika mstari wa 13 na endelea kusoma hadi mwisho wa kifungu hiki. Je uliona ushauri uliotolewa kwa watu wa Musa “Usiogope, simama tu na mkauone wokovu wa Bwana”.

Angalia katika Waraka wa kwanza wa Yohana sura ya 4 mistari ya 15 hadi 19. Mstari wa 15 unawataka wale wote ambao wamekuwa wakifikiria juu ya ubatizo lakini kwa hakika bado hawajaamua. Iwapo tumo “ndani ya Yesu” tumezungukwa na Upendo wake wa hakika na kwamba Upendo wa kweli unaondosha hofu.

Kuna maneno mengine ya ajabu na ya kuliwaza katika Zaburi 34; jaribu kuisoma Zaburi hii. Haya yanaweza kubadilisha msimamo wetu juu y maisha; Angalia kwa makini mistari ya 4 hadi 8. Katika mstari wa 9 wa Zaburi hii, tunapewa mawazo mapya, ikiwa hofu itakuwepo katika maisha yetu basi iwe hofu ya tofauti, iliyo bora, hofu ambayo ni nzuri kwetu hofu ya Bwana Mungu.

Ukisoma mstari wa 11 utakuta wito ulioandikwa na Daudi mtungaji wa Zaburi. Alikuwa ni mtu ambaye wakati wa ujana wake aliondoka kwenda kupigana na jitu la Filisti Goliati, kiwa na kombeo tu na mawe machache madogo hali akiwa na imani kuu kwa Mungu wake.

Daudi anatupa ushauri mzuri, hofu ya Mungu ni safi na ni nzuri kwetu sisi. Hii ina maana kuwepo kwake. Daima tutamuheshimu Mungu na kutambua jinsi alivyokaribu nasi kupitia Malaika wake.

Mambo tuyafanyayo katika maisha yetu yatakuwa ya uaminifu na mazuri na kama tunavyompenda Mungu ndivyo tutakavyoona rahisi kuwapenda jamaa zetu kama alivyofanya Yesu. Kumbuka hata wakati alipokuwa anasulubiwa msalabani akiwa katika maumivu makali mno, alimwomba Baba yake kusamehe. “Baba Uwasamehe kwani hawajui watendalo.”

Mtume Yohana anatueleza mengi juu ya Upendo katika maisha yetu lakini pia anatumbia juu ya hofu ya Mwanadamu na hii ndiyo sehemu nzuri ya kumalizia.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)